CHAMA CHA WAFANYAKAZI WA TAASISI ZA ELIMU YA JUU
Website: http://thtu.biz.tc

# YAJUE MANUFAA YA THTU

## Kwa kujiunga na THTU mwanachama atapata manufaa yafuatayo:

➔ Punguzo la ada ya mwanachama toka asilimia mbili kwenda 1%
Ada haitazidi Tshs **20,000** hata kama 1% ya mshahara ikiwa kubwa zaidi.

➔ Mwanachama wa THTU anaendelea kuhudumiwa na chama hata baada ya kustaafu.
Chama kitafuatilia mafao ya wastaafu wasinyayaswe juu ya mafao yao. Chama pia kitaendelea kutetea maboresho ya mafao hayo.

➔ Wanachama wote wa THTU wana haki sawa kutetewa na wanapata heshima sawa bila kujali ni wafanyakazi waendeshaji au wanataaluma.
THTU imebatilisha dhana ya kubagua wafanyakazi kwenye makundi ya watafiti, wanataaluma na wengineo jambo lililosababisha wafanyakazi waendeshaji kukosa haki yao ya nyongeza ya mishahara kama kamati ya Rais ya 2005 ilivyopendekeza.

➔ Mwanachama wa THTU ngazi ya tawi ana nafasi ya kukiwakilisha chama ngazi ya kanda na Taifa ili mradi tu amechaguliwa na wanachama wa tawi lake kuwa mwakilishi.
Idadi ya wawakilishi kanda na Taifa inategemea tu idadi ya wanachama katika tawi husika

➔ Mwanachama wa THTU ana nafasi ya kushiriki kikamilifu katika maamuzi yote ya chama ngazi ya tawi, kanda, hadi taifa.
Kiongozi wa THTU ngazi yoyote anaweza kuondolewa kwa kura/maamuzi ya wanachama ngazi ya Tawi ambalo anatoka kama kiongozi huyo atakiuka misingi na katiba ya chama chake.

➔ Mwanachama wa THTU ana nafasi nzuri ya kujiendeleza kiufundi/kikazi au kitaaluma kwa kutumia nafasi za masomo zitakazotolewa na chama chake.
Chama cha THTU kina mpango wa kuwasaidia wafanyakazi waliokwama ngazi moja kwa kuwapa uwezekano wa kujiendeleza kimasomo.